# MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: COVID-19 KATIKA MUKTADHA WA KULAZIMIKA KUKIMBIA MAKAZI: UZOEFU_KUTOKA MASHARIKI YA KATI NA AFRIKA MASHARIKI.

Katika Mashariki ya Kati na Afrika Mashariki, COVID-19 imeongeza mazingira hatarishi ambayo tayari wanayapitia watu waliolazimika kukimbia makazi yao kutokana na vita (wakimbizi, watafuta hifadhi, watu waliokimbia makazi yao nchini mwao na wasio na uraia). Pamoja na hatari kubwa ya kiafya kutokana na janga la gonjwa hili, hatua za vizuizi vya kutoka nje zilizowekwa na serikali kupunguza kuenea ugonjwa zimekuwa na madhara ya kupitiliza kwa watu waliolazimika kukimbia makazi yao, kuongeza umaskini, chuki dhidi ya wageni na kusababisha masuala mapya ya ulinzi wa kibinadamu.

Jarida hili la muhtasari linatoa maoni juu ya njia ambazo watoa misaada ya kibinadamu, asasi au mashirika ya kiraia na idara za serikali zilizo na majukumu maalumi kwa watu waliokimbia makazi yao zinaweza kuchangia kupunguza mazingira hatarishi katika janga la gonjwa hili, ambayo tunayazungumzia hapo chini. Kwa maoni na maelezo ya kina zaidi kuhusu miitikio mahalia ya COVID-19 kwa watu waliolazimika kukimbia makazi yao Mashariki ya Kati na Afrika Mashariki, angalia Andiko letu kamili: COVID-19 katika muktadha wa kulazimika kukimbia makazi: Uzoefu kutoka Mashariki ya Kati na Afrika Mashariki.

## MUHTASARI WA MAONI

### Tumia miitikio jumuishi

- Migogoro ya muda mrefu huko Palestina, Lebanon, Iraq na Syria, pamoja na Sudan Kusini, Somalia na mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imebadilisha kwa kiasi kikubwa namna watu wanavyohama makazi huko Mashariki ya Kati na Afrika Mashariki tangu vizazi na vizazi, ikiathiri mbinu za kukabiliana na hali kwa watu wanaoamua kuondoka na wale wanaobaki.
- Miitikio ya COVID-19 inapaswa kutambua vyanzo mbalimbali vya mateso ambavyo watu waliolazimika kukimbia makazi yao tayari wameyapata na kuhakikisha kwamba watu waliokimbia makazi yao hawasukumwi katika hali ya hatari zaidi kutokana na hatua za afya ya umma.
- Watoa misaada ya kibinadamu, asasi za kiraia na idara za serikali zinaweza kupunguza hali hatarishi katika janga la gonjwa hili si tu kwa kusaidia mifumo ya afya kukabiliana na COVID-19, bali pia kwa i) kukubali programu za kudumisha huduma muhimu, ii) kushirikiana na


Anwani ya barua pepe a.wilkinson@ids.ac.uk

serikali kuepuka kuweka hatua za kudhibiti COVID-19 ambazo hazizingatii haki ambazo zinawaumiza watu walioko tayari katika mazingira hatarishi, na iii) kuwasaidia watu waliolazimika kukimbia makazi yao kushinda vizuizi vya kimuundo na kuchukua chukua majukukumu makubwa zaidi ya miitikio dhidi ya ya COVID-19.

### Shirikiana na vikundi mahalia

- Watoa misaada ya kibinadamu wanaokabiliana na COVID-19 wanapaswa kuzingatia aina mahsusi na mazingira mbalimbali ya watu waliolazimika kukimbia makazi yao wanayoyaishi wakati wa kukimbia, pamoja na njia mbalimbali za kuhama. Mara nyingi, maeneo ambayo watu waliolazimika kukimbia makazi yao hukaa huwa maeneo ya mamlaka mchanganyiko. Programu za misaada ya kibinadamu, mashirika ya kidini, kamati za wazee na mahakama za jadi, vyama vya siasa na asasi za kiraia na vyama vya ndani vya ushirika wa kifedha vinaendesha shughuli zao kwa pamoja, vikitoa fursa mbalimbali za uongozi na ushiriki, ikiwemo kushirikiana na afua za afya ya umma.
- Kuhusisha raia wanaoishi nje ya nchi na makundi yanayoongozwa na wakimbizi wenyewe linaweza kuwa jambo lenye umuhimu wa kipekee la kuboresha usaidizi kwa watu waliokimbia makazi ambao hawaishi kwenye makazi rasmi.
- Mashirika ya misaada ya kibinadamu yanapaswa kuwekeza katika kuelewa mifumo ya ndani ya kijamii na utoaji misaada, kutengeneza mahusiano nayo, na kusaidia watu kubaini vipaumbele vya ndani, kufuatilia matatizo na kusaidia kuandaa utatuzi.
- Tahadhari inapaswa kuchukuliwa ili kuelewa makundi hayo mbalimbali yanamwakilisha nani, mawazo ya watu gani yanaweza yasizingatiwe katika mifumo hii na namna mikakati inavyoweza kuchukuliwa ili kuakisi utofauti wa watu waliolazimika kukimbia makazi yao ndani na nje ya mipaka.

### Epuka kuweka vizuizi vya jumla vya kutoka nje ambavyo vinatishia usalama wa kiuchumi

- Watu waliokimbia makazi yao huwa wana uwezekano wa kuwa sehemu ya mitandao ya jamii inayohusisha nchi mbalimbali inayochangiana kipato, misaada na fursa nyingine za kujikimu kimaisha ili kukabiliana na majanga mbalimbali. Hata hivyo, mahusiano haya ya kijamii na rasilimali, yanapitia hali ngumu kutokana na vizuizi vya kusafiri na kuendesha biashara kama sehemu ya mapambano dhidi ya COVID-19 (vizuizi vya kutoka nje):
  - Watu wengi waliokimbia makazi yao wanaishi makambini na makazi ya muda ya mjini yasiyo rasmi wanategemea ujira wa kila siku na wana akiba na mafao ya ajira kidogo kuweza kuhimili ugumu utokanao na vizuizi vya ajira.
  - Hasa Afrika Mashariki, maagizo ya kukaa nyumbani pia yanatishia uwezo wa watu waliokimbia makazi yao na wale walio kwenye mitandao yao ya jamii wa kulima na kuzipatia chakula familia zao. Watu wengi walioko makambini wanapitia hali ya kupunguziwa misaada ya kibinadamu kwa sababu ya athari za kifedha duniani kote kutokana na ja janga la gonjwa hili na wengi walioko nje ya makambi hawawezi kupata msaada wa kifedha kutoka serikalini.


Anwani ya barua pepe: a.wilkinson@ids.ac.uk

- Kila inapowezekana, watoa misaada ya kibinadamu na watendaji wa ndani wanapaswa kufanya kazi na idara za serikali kuepuka kuweka vizuizi vya jumla vya kutoka nje ambavyo vinaumiza zaidi shughuli za kujikimu za watu waliokimbia makazi yao. Kwa mfano, taratibu zisizowabana sana watu kama vile kukaa mstarini na kupeana zamu za siku kwa wachuuzi binafsi zinaweza kusaidia kudumisha umbali salama kati ya mtu na mtu katika masoko ya wazi ambako biashara inafanyika.
- Watu waliokimbia makazi hawapaswi kuchukuliwa kabisa kama 'wategemea misaada' au 'wanaojitegemea' tu. Wafadhili wa kimataifa wanapaswa kuendelea kutoa kwa ukarimu kwa mifumo ya misaada ya kibinadamu ili kuunga mkono watu waliokimbia makazi yao katika mazingira magumu ya kiuchumi. Watoa misaada ya kibinadamu na watendaji wa ndani wanapaswa kuwekeza katika mifumo ya dharura ya uhakika wa kifedha ambayo inaweza kuwafikia wakimbizi waliojenga makazi yao wenyewe wakati wa hali ngumu.

### Kupunguza makali ya athari za ulinzi wa upimaji na ufuatiliaji

- Haki za watu waliokimbia makazi za kuvuka mipaka na kusafiri nje ya makambi mara nyingi inaminywa kwa urasimu jambo ambalo linawaweka katika hatari ya kufanyiwa ukatili na kunyang'anywa fedha na polisi na vyombo vya usalama. Kama maeneo yanayoonekana kirahisi wanayoishi watu waliokimbia makazi yao, makambi na mipaka yake yamewekwa chini ya uangalizi wa kiafya, kiusalama na kijamii wakati wa janga la gonjwa hili ambao umeongeza chuki dhidi ya wageni na kuchangia kuwekwa kwa hatua zisizozingatia usawa za vizuizi vya kutoka nje kwa watu waliolazimika kukimbia makazi yao.
- Serikali na watoa misaada ya kibinadamu wanaokabiliana na COVID-19 wanapaswa kuweka uwiano mzuri kati ya haja ya kudhibiti kuenea ugonjwa na kudumisha haki za hifadhi na huduma muhimu kwa watu waliokimbia makazi yao.
- Wakimbizi wasiosajiliwa wanapaswa kupewa msamaha wa muda wa kupata huduma za afya bila ya kuwaweka wakimbizi hao katika hatari ya kukamatwa au kurejeshwa makwao.
- Wanausalama wanapaswa kufuatilia kuzuka kwa shughuli za vikundi vya ulinzi visivyo rasmi ili kupunguza uwezekano wa kukamatwa kwa wahamiaji haramu walioko katika mazingira yasiyo salama au kushambuliwa na makundi ya watu kinyume cha sheria kwa wale wanaoonekana kuhatarisha usalama wa makambi na kutangaza fursa salama, mbadala kwa wanaotafuta hifadhi kujisajili.
- Kwa kuwa mizozo inayohusiana na usafi binafsi ni mbinu ya kawaida inayotumika na pande zinazopigana kukuza uhasama na vikundi vya maadui, programu za elimu ya COVID-19 zinapaswa kuchukua tahadhari kutowanyanyapaa bila kukusudia watu waliokimbia makazi yao kwa kutia chumvi maelezo kuhusu ugonjwa yanayohusiana na kusafiri au vikundi fulani.

### Usiwatake watu kuondoka majumbani kwao wakati wa mlipuko

- Watu waliolazimika kukimbia makazi yao huelekea kuishi katika hali hatarishi zaidi kuliko watu wanaowazunguka. Ardhi iliyotengwa kwa ajili ya makambi ya miitikio ya kibinadamu au inayopatikana kwenye makazi yasiyo rasmi ya mijini inaweza isitoshe, na kusababisha


Anwani ya barua pepe: a.wilkinson@ids.ac.uk

msongamano na kuongeza mazingira hatarishi ya watu waliokimbia makazi yao kueneza COVID-19.

- Makambi na makazi yasiyo rasmi yanaweza pia kuhusishwa na mizozo ya kisiasa, na mara kwa mara kutishiwa kufungwa. Wakati wa janga la gonjwa la COVID-19, baadhi ya watu walioko makambini Afrika Mashariki na Mashariki ya Kati wameshauriwa 'kurejea makwao' hata pale inapokuwa si salama kufanya hivyo.
- Msongamano wa watu usitumike kama kisingizio cha kuondoa watu makambini, hasa wakati wa janga ambapo watu wengine walioko katika mitandao ya jamii ya watu waliokimbia makazi yao wana rasilimali chache zaidi za kusaidia watu wasio na makazi. Watoa misaada ya kibinadamu na watendaji wa serikali sharti walinde nyumba za watu zilizopo na kuhakikisha zinakuwa salama.

## Linda upatikanaji wa kawaida wa huduma ya afya

- Watu waliokimbia makazi wa rika zote huelekea kuwa na afya mbaya kuliko watu ambao hawajakimbia makazi yao, ikiwemo maradhi sugu ambayo hayajapatiwa matibabu hali ambayo inawafanya wawe katika hatari zaidi ya kuathirika zaidi kutokana na COVID-19.
- Katika baadhi ya maeneo, vizuzi vya kusafiri vinazuia upatikanaji wa huduma za afya. Watendaji wa serikali wanapaswa kuhakikisha msamaha unaohusiana na kutafuta tiba ya afya na uamuzi utokanao na jambo hilo kutolewa taarifa polisi na umma.
- Katika mifumo ya afya iliyovurugika au kubinafsishwa sana, hospitali za serikali huelekea kuwapokea watu waliokimbia makazi yao na aina hii hii ya vituo pia vimelengwa kwa upendeleo wa afua za kitaifa dhidi ya COVID-19. Wakati wa kuomba kuongezewa rasilimali kwa shughuli za mifumo ya COVID-19, watoa misaada ya kibinadamu na mamlaka za serikali sharti walinde haki ya watu waliokimbia makazi yao na uwezo wa kupata huduma huko. Wanapaswa kuepuka kuvitoa vituo hivyo vya afya moja kwa moja kwa mwitikio kwa vile kutafuta matibabu ya magonjwa mengine kwingineko itakuwa nje ya uwezo wa kifedha wa wengi wa watu waliokimbia makazi yao.
- Programu za misaada ya kibinadamu sharti ifikirie kutumia au kupanua mifumo ya msingi wa kijamii ya huduma za matibabu ili kudumisha shughuli muhimu za kukinga na huduma kwa watu waliokimbia makazi yao wenye maradhi sugu kupunguza uzito wa kazi kwenye vituo vya afya.

## Dumisha juhudi za kuleta amani

- Licha ya miito ya kimataifa ya kusitisha mapigano katika migogoro inayoendelea kuwezesha kudhibiti ugonjwa wa COVID-19, vita nyingi Mashariki ya Kati na Afrika ya Mashariki havijakoma.
- Wakati vizuizi vya kimataifa vya kusafiri vinaendelea, ni muhimu kwamba wanadiplomasia wachukue taratibu ambazo zitadumisha juhudi za kuleta amani. Hii inajumuisha kujenga uwezo wa kimataifa na ndaniwa amani na kuunga mkono juhudi za kimataifa za kusitisha vita ili kuzuia wahamiaji wapya. Watendaji hawa wanapaswa pia kudumisha njia za misaada


Anwani ya barua pepe: a.wilkinson@Ids.ac.uk

ya kibinadamu ili kusaidia katika mapambano dhidi ya COVID-19 na kuwezesha watu walioathiriwa na migogoro kupata huduma za afya.

**Punguza vizuizi vya ujumuishwaji wa watu waliolazimika kukimbia makazi yao katika utoaji maamuzi dhidi ya COVID-19**

- Miitikio mingi dhidi ya COVID-19 inayofanywa na watu waliokimbia makazi yao, watoa misaada ya kibinadamu na serikali imenufaika na uzoefu na utaalamu wa watendaji wa ndanikukabiliana na migogoro ya kisiasa katika utoaji misaada na kuepusha kuvurugika kwa mfumo wa afya.
- Taratibu muhimu za kisheria na za kawaida za serikali za jumuiya za wenyeji, vyama vya kitaaluma na washirika wa misaada ya kibinadamu hata hivyo zinakwamisha zaidi ujumuishaji wa wakimbizi na IDP katika kutoa maamuzi kwenye ngazi zote. Kwa mfano, mashirika ya wakimbizi mara nyingi hayajahusishwa katika vikosi kazi vya mwitikio dhidi ya COVID-19. Jambo hili linapunguza uwezo wa miitikio dhidi ya COVID-19 kuboresha mazingira hatarishi kupitia 'utaratibu unaohusisha jamii nzima', kama ilivyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani.
- Upekee wa janga la gonjwa la COVID-19 unatoa fursa ya kipekee kwa serikali na watoa misaada ya kibinadamu kushirikiana na wahamasishaji ili kuondoa baadhi ya vizuizi vya kisheria, taratibu za kifedha na desturi za kijamii ambazo zinazuia ujumuishwaji zaidi wa watu waliokimbia makazi yao katika kutoa maamuzi ambayo yanabadilisha mazingira yao hatarishi kwa janga la gonjwa hili na majanga mengine ya kibinadamu.


Anwani ya barua pepe: a.wilkinson@Ids.ac.uk

## MAWASILIANO

Kama una ombi la moja kwa moja kuhusiana na mwitikio dhidi ya COVID-19, kuhusu maelezo, zana, utaalamu wa ziada wa kiufundi au uchambuzi kwa masafa, au kama ungependa kufikiriwa kujiunga na mtandao wa washauri, tafadhali wasiliana na Social Science in Humanitarian Action Platform kwa kuandika barua pepe kwenda kwa Annie Lowden (a.lowden@ids.ac.uk) au Olivia Tulloch (oliviatulloch@anthrologica.com). Sehemu muhimu za mawasiliano ya Platform hii ni pamoja na: UNICEF (nnaqvi@unicef.org); IFRC (ombretta.baggio@ifrc.org); na GOARN Research Social Science Group (nina.gobat@phc.ox.ac.uk).

The Social Science in Humanitarian Action ni ubia kati ya Institute of Development Studies, Anthrologica na London School of Hygiene and Tropical Medicine. Fedha za kuuunga mkono mwitikio wa Shirika hili dhidi ya COVID-19 zimetolewa na Wellcome Trust na DFID. Maoni yaliyotolewa ni ya waandishi wenyewe na si lazima kwamba yanawakilisha maoni au sera za IDS, Anthrologica, LSHTM, Wellcome Trust au serikali ya Uingereza.

Mapendekezo ya nukuu: Duclos, D. and Palmer, J. (2020) 'Key Considerations: Covid-19 in the Context of Forced Displacement – Perspectives from the Middle East and East Africa', *Briefing*, Brighton: Social Science in Humanitarian Action (SSHAP)

Kimechapishwa Julai 2020

© Institute of Development Studies 2020

Hili ni andiko la Wazi linalosambazwa chini ya vigezo vya Creative Commons Attribution 4.0 International licence (CC BY), vinavyoruhusu matumizi, usambazaji na uzalishaji usio na masharti kwenye mfumo wowote wa mawasiliano, ilimradi tu kwamba waandishi halisi na vyanzo vinatajwa na mabadiliko yoyote au kutumika vinginevyo kunatajwa. http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/legalcode